**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

**MHE. MWENYEKITI NA WAJUMBE,**

**BARAZA LA MADIWANI.**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA.**

IMC

**TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA) MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 02/12/2020**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mhe. Mwenyekiti**, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya Mwaka. Hivyo, taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-

i. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati Nyamhongolo.

ii. Taarifa ya Utekelezaji wa miradi mipya itakayotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia programu ya Tanzania Cities Transforming Infrastructure Competitiveness – TACTIC (yaani Mradi wa kuendeleza miundombinu na ushindani katika Majiji, Manispaa na Miji ya Tanzania)

iii. Taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba na Darasa la Nne wa Mwaka, 2020.

iv. Taarifa ya Maandalizi ya Mtihani wa Kidato cha Pili na cha Nne Mwaka 2020.

v. Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2020.

vi. Taarifa ya Halmashauri kupata Hati Safi katika Hesabu za Mwaka wa Fedha 2019/2020.

vii. Taarifa ya kuvunja Mkataba na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika mradi wa Jengo la Utawala katika Makao Makuu ya Halmashauri.

viii. Taarifa ya kuanza kwa huduma ya upasuaji katika Kituo cha Afya Buzuruga.

ix. Taarifa ya tukio la moto katika Shule ya Sekondari Loreto.

x. Taarifa ya Maandalizi ya mapokezi ya Wanafunzi wa Darasa la kwanza kwa Mwaka 2021.

xi. Taarifa ya Maandalizi ya mapokezi ya Wanafunzi wa Kidato cha kwanza kwa Mwaka 2021.

xii. Kupokea taarifa za Utekelezaji wa Shughuli za Halmashauri katika kipindi cha robo ya kwanza kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Taarifa za miradi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## 2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

### *2.1 Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati Nyamhongolo.*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri inaendelea na utekelezaji wa miradi miwili ya kimkakati ya ujenzi wa Maegesho ya Malori na ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika eneo la Nyamhongolo kwa gharama ya Tshs. 27,095,103,464.00. Hadi sasa miradi hiyo yote miwili imefikia hatua ya utekelezaji ya wastani wa asilimia 60%.Mpaka sasa Halmashauri imepokea na kulipa Mkandarasi pamoja na Mtaalam Mshauri jumla ya kiasi cha Tshs. 9,353,216,743.63. Maendeleo ya miradi yote kwa ujumla ni mazuri na Mkandarasi yupo anaendelea na kazi kwa kasi nzuri inayoashiria kuwa atamaliza kutekeleza miradi yote miwili ndani ya

IMC

muda uliopangwa (Mwezi Mei,2021 kwa mujibu wa Mkataba). Hata hivyo, hii itategemea na mtiririko wa Fedha iwapo utaenda vizuri.

### *2.2 Taarifa ya Utekelezaji wa miradi mipya itakayotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia programu ya Tanzania Cities Transforming Infrastructure Competitiveness – TACTIC (yaani Mradi wa kuendeleza miundombinu na ushindani katika Majiji, Manispaa na Miji ya Tanzania)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri inaendelea na hatua za awali za utekelezaji wa miradi mikubwa ya:-

- Ujenzi wa Soko la kisasa Kirumba pamoja na barabara zinazozunguka Soko zenye urefu wa kilomita 2.5 zitajengwa kwa kiwango cha lami;
- Ujenzi wa barabara za kiwango cha lami Buswelu – Busenga – Cocacola - Igoma yenye urefu wa Kilomita 3.3;
- Barabara ya Buswelu – Nyamhongolo (Mbogamboga – Nyamadoke – Nyamhongolo Bus terminal) yenye urefu wa Kilomita 9.25; na
- Ujenzi wa barabara ya Pasiansi- Lumala – Kiseke PPF Kilomita 3.25.

Miradi yote hii itatekelezwa na Serikali ya Jamhuri wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ambapo hatua ya Upembuzi yakinifu inaendelea kwa ajili ya kuandaa michoro na usanifu (Feasibility Study and Detailed Design)

Vilevile, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kupitia mradi wa DSDP itanufaika kwa kujengwa kwa mto unaotiririsha maji katika maeneo ya mto Mayolwa Kata ya Ibungilo (Msuka), Kona ya Bwiru, Kitangiri na Kirumba.

Aidha, Mradi huu unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia programu ya DSDP, mpaka sasa Mtaalam Mshauri amemaliza kazi ya kuandaa michoro na usanifu na hatua iliyofikiwa serikali inaendelea taratibu za kutoa idhini ili hatua za Manunuzi kupitia OFISI YA RAIS – TAMISEMI ziendelee.

IMC

## 2.3 Taarifa ya Mtihani wa Darasa la Nne na Darasa la Saba kwa Mwaka 2020

### 2.3.1 Mtihani wa Darasa la Saba

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Napenda kulitaarifu Baraza lako kuwa, mnamo tarehe 07 – 08/10/2020, jumla ya wanafunzi 10,145 wa Darasa la saba katika Shule za Msingi 118 zilizopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela walifanya Mtihani wa kumaliza Darasa la saba. Kati ya shule hizo zenye wanafunzi wa darasa la saba, za Serikali ni 75 na binafsi ni 43.

Mtihani ulifanyika kwa amani na usalama na hakukuwa na changamoto kubwa na matukio mabaya yaliyojitokeza.Hii inatokana na Kamati kujipanga vizuri katika kusimamia zoezi hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Mitihani limetoa matokeo ambapo jumla ya wanafunzi 9,869 wamefaulu mtihani huo sawa na asilimia 97.28%. Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika matokeo hayo imeshika nafasi ya sita kitaifa na nafasi ya pili Kimkoa ambapo imeshuka kutoka nafasi ya Pili Kitaifa na nafasi ya kwanza Kimkoa Mwaka, 2019.

### 2.3.2 Mtihani wa Darasa la Nne

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Vilevile, wanafunzi wa darasa la nne wapatao 12,461 walifanya Mtihani wa upimaji wa kitaifa tarehe 25 – 26/11/2020 katika Shule za Msingi 125 zilizopo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Mtihani ulifanyika kwa amani na usalama na hakuna changamoto kubwa na matukio mabaya yaliyojitokeza hadi mtihani ulipokabidhiwa ngazi ya Mkoa.

## 2.4 Taarifa ya Mtihani wa Kidato cha Pili na cha Nne wa Mwaka 2020

### 2.4.1 Mtihani wa Kidato cha Pili

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** napenda kulitaarifu Baraza lako kuwa, mnamo tarehe 09–20/11/2020, wanafunzi wa kidato cha pili walifanya mtihani wa

IMC

upimaji katika Halmashauri yetu na jumla ya shule 49 za Sekondari zikiwemo shule 26 za Serikali na shule 23 za binafsi. Idadi ya watahiniwa wa kidato cha pili kutoka shule zote walikuwa 8,087 ambapo katika kipindi chote mtihani ulifanyika kwa hali ya usalama na amani. Aidha, mtihani huo tayari umekabidhiwa ngazi ya Mkoa.

### 2.4.2 Mtihani wa Kidato cha Nne

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kama ilivyokuwa kwa madarasa mengine ya mitihani tarehe 23/11/2020 hadi 11/12/2020 jumla ya watahiniwa (wanafunzi) ni 6,761 wa kidato cha Nne wanaendelea na Mitihani katika shule 45 za sekondari zilizopo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

### *2.4.3 Taarifa ya matokeo ya kidato cha sita, Mwaka 2020*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kulitaarifu baraza lako kuwa katika matokeo ya kidato cha sita Mwaka 2020 shule yetu kongwe ya Bwiru Wasichana ilifanya vizuri katika matokeo wa kidato cha sita. Shule hii imekuwa ya nne kimkoa kwa ufaulu mzuri na hapakuwa na daraja sifuri kwa watahiniwa wote ikilinganishwa na Mwaka 2019 ambapo Kimkoa ilikuwa ya 29.

Hivyo, niwaombe wajumbe mnapoanza majukumu yenu wahimizeni wananchi kuwasimamia watoto wetu katika kuzingatia masomo. Wakati huohuo wajitoe katika kuchangia shughuli za maendeleo hususani ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika shule zetu.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutoa Fedha kiasi cha Tsh. 1,800,818,115.20 kukarabati shule kongwe katika halmashauri matunda yake ndiyo tunayoyaona leo.

## 2.5 Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 20202.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa mujibu wa Ibara ya 38 na 39 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (kama ilivyorekebishwa)

IMC

inaweka masharti ya kufanyika uchaguzi wa kiraia kila baada ya miaka mitano.Hivyo, mnamo tarehe 28/10/2020 Taifa letu lilifanya Uchaguzi Mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge na Madiwani. Katika uchaguzi huo kwa upande wa Jimbo la Ilemela jumla ya Vyama vya Siasa 15 vilishiriki uchaguzi ambapo wagombea wa nafasi ya Rais walikuwa 15, wagombea wa nafasi ya Ubunge walikuwa 7 na Wagombea wa nafasi ya Udiwani walikuwa 50. Matokeo ya Uchaguzi huo katika Jimbo la Ilemela yaliupatia ushindi mkubwa Chama Cha Mapinduzi ambapo kilishinda nafasi ya Rais kwa asilimia 91%, nafasi ya Ubunge kwa asilimia 83.9% na Madiwani katika kata zote 19 walishinda kwa ushindi wa kishindo (landslide victory).

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kutoa pongezi nyingi za dhati kwa wajumbe wote wa Baraza hili la Madiwani kwa ushindi huo mkubwa na sasa karibuni sana tuendelee kuijenga Ilemela kwa kauli mbiu iliyoasisiwa na Mhe.Diwani mwenzenu katika kipindi kilichopita cha awamu ya kwanza ya utawala wa awamu ya tano ambaye ni Mbunge wa Jimbo hili la Ilemela isemayo "***ILEMELA NI YETU TUSHIRIKIANE KUIJENGA"*** kauli mbiu imekuwa ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo tuliyoyapata katika kipindi cha Mwaka 2015-2020. Mwenye macho haambiwi tazama, kwani maendeleo yaliyofikiwa yanaonekana na kupimika bila hata kutumia nadharia za kisayansi. Mathalani, kivuko cha Kayenze –Bezi-Bukimwi Ukerewe, Barabara za kiwango cha lami, Miradi ya Kimkakati Nyamhongolo, Uendelezaji wa makazi kupitia Sekta ya ardhi, Ujenzi wa miundo mbinu ya Shule za Msingi na Sekondari (tumefungua shule tatu za Sekondari na shule mbili za Msingi) n.k

## 2.6 Taarifa ya Halmashauri kupata hati safi Hesabu za Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** napenda kuchua fursa hii kulitaarifu Baraza lako la Madiwani kuwa, Katika ukaguzi uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Halmashauri yako imepata Hati Safi. ***Mafanikio haya yalitokana na***

***usimamizi wako imara kupitia baraza lililopita (2015-2020)*** Hii inadhihirishwa na matokeo ya kaguzi zilizofanyika kwa vipindi vya nyuma tangu Baraza la Madiwani lianze kwa awamu ya kwanza ya utawala wa awamu ya tano 2015-2020, Halmashauri imekuwa ikipata **HATI SAFI** kwa miaka mitano mfululizo**.**

Mafanikio haya yanatokana na ushirikiano, uadilifu na uwajibikaji wa pamoja baina ya Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Halmashauri katika ngazi zote. Timu ya Menejimenti inaahidi kuongeza bidii kwa kufanya kazi bila kuchoka ili kuyalinda mafanikio kwa kuhakikisha inatoa ushirikiano, kuwa na uadilifu na uwajibikaji wa kiwango cha juu katika kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wa Ilemela na Watanzania kwa ujumla kwa kuzingatia raslimali zitakazokuwepo.

### 2.7 Taarifa ya kuvunja Mkataba na Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) katika Mradi wa Jengo La Utawala.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela iliingia Mkataba na TBA katika mradi wa jengo la utawala kuanzia Mei, 2018 hadi Mei, 2019. Kazi ya ujenzi wa mradi huo ilisimama tangu Januari, 2019 kutokana na kusuasua kwa mtiririko wa Fedha za utekelezaji wa mradi kulingana na masharti ya Mkataba.

Kufuatia hali hiyo, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ilipofanya ziara yake ya kikazi katika Halmashauri yako mnamo tarehe 19/03/2019 pamoja na mambo mengine kamati ilifanya ukaguzi wa miradi iliyokuwa ikitekelezwa ilibaini kwamba mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala ulikuwa umesimama na Mkandarasi haendelei na ujenzi. Kamati hiyo ilitoa maagizo kuwa Halmashauri ivunje Mkataba na TBA kutokana na kushindwa kuendelea na kazi. Timu ya Menejimenti iliitisha kikao na TBA Septemba, 2020 ili kukubaliana namna ya kuvunja mkataba na pande zote ziliafikiana Mkataba uvunjwe ili kuendelea na hatua zingine za kupata Fedha kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi kwa njia ya 'Force Account' kama ambavyo ilishauriwa

na Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha. Makubaliano hayo ya kuvunja Mkataba yaliandaliwa na kusainiwa upande wa Halmashauri kisha kupelekwa TBA kwa ajili ya kusainiwa upande wake hatua ambayo bado hadi sasa haijatekelezwa. Halmashauri kwa sasa imeendelea na taratibu za kuomba Fedha za mradi huo kutoka Wizara ya Fedha ili mradi uendelee kutekelezwa kwa njia ya ''Force Account" na tayari maombi yamewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza.

### ***2.8 Taarifa ya kuanza kwa huduma ya upasuaji akina mama wajawazito katika kituo cha afya Buzuruga***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kushirikiana na Taasisi ya AGHAKAN FOUNDATION imekamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo cha afya Buzuruga kwa gharama ya Tsh. 173,055,995.00. Baada ya jengo hilo pamoja na vifaa tiba kukamilika huduma ya upasuaji ilianza kutolewa tarehe 06/11/2020 na hadi sasa idadi ya wamama wajawazito 12 wamefanyiwa upasuaji na wote wanaendelea vizuri. Changamoto iliyokuwepo ya upungufu wa dawa na baadhi ya vifaa vifaa tiba pamoja na standby generator ofisi yangu (Mkurugenzi) tayari imezishughulikia kwa kutoa Fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaaa tiba na genereta. Hatua za manunuzi zinaendelea.

### ***2.9 Taarifa ya tukio la moto katika shule ya sekondari Loreto***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 21/11/2020, saa 12:20 jioni kulitokea janga la moto katika moja ya Mabweni ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Loreto iliyopo Mtaa wa Majengo Mapya, Kata ya Nyakato. Moto huo ulianzia kwenye ghorofa ya pili ambayo wanaishi wanafunzi wa kidato cha Kwanza wapatao 185 kati ya wanafunzi 351 wanaoishi kwenye bweni hilo lililoungua moto. Jitihada za kuzima moto zilifanyika kupitia Jeshi la Zimamoto kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi.

Mhe.Mwenyekiti, hakuna Mtoto au Mtumishi wa shule hiyo aliyejeruhiwa au kupoteza maisha kutoka na tukio hilo. Hata hivyo, zipo athari zilizojitokeza kwenye maafa hayo ambapo wanafunzi wa Kidato cha kwanza wapatao 185 vifaa vyao vyote viliteketetea kwa moto pamoja na miundombinu ya bweni kuharibika. Kwa sasa wanafunzi wote 351 waliokuwa wakiishi kwenye jengo lililoungua, wamehamishiwa kwenye bweni lingine wakati vyombo vinaendelea na uchunguzi wa tukio.

Mhe.Mwenyekiti, ninaomba kulifahamisha Baraza lako kuwa Halmashauri yako kupitia Jeshi la Zimamoto haina vyombo madhubuti vya kupambana na majanga ya aina hii pindi yanapotokea, hususani magari kwani yaliyopo yote yalirithiwa na iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ambayo ni machakavu kutokana na kuwa ni ya muda mrefu. Kupitia mkutano huu wa kwanza wa Baraza ninaomba kutoa rai kuipatia ufumbuzi changamoto hii kwa siku zijazo maana eneo la Halmashauri yako linazidi kukua kutokana na shughuli za kiuchumi kuongezeka kila uchao.

## 2.10 Taarifa ya Maandalizi ya mapokezi ya Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kwa Mwaka 2021.

Mhe.mwenyekiti, ninaomba kulifahamisha Baraza lako kuwa ifikapo Januari, 2021. Halmashauri inatakiwa kuhakikisha watoto wote wanaostahili kuanzishwa darasa la awali na la kwanza katika shule zetu za umma za Msingi na waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule zetu za umma za Sekondari wanapata madarasa na madawati na viti na meza.

Kwa upande wa Sekondari matarajio ya idadi ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza ni 7493 ikiwa kati yao Wasichana ni 3,888 na wavulana 3,605. Kwa idadi hiyo, Vyumba vya madarasa vilivyopo kwa ajili ya kidato cha kwanza ni 85 kati ya mahitaji ya vyumba 150, hivyo vyumba 65 vinahitajika. Mhe. Mwenyekiti itakumbukwa katika kipindi cha Baraza lililopita Halmashauri kwa kushirikiana na Mbunge, Wananchi kupitia

Waheshimiwa Madiwani na ofisi ya Mkuu wa Wilaya wananchi walihamasishwa kujenga misingi na ofisi ya Mbunge ilitoa matofali kupitia Mfuko wa Jimbo na Halmashuri yako ilikamilisha Madarasa. Mpaka sasa ipo misingi 61 na maboma ya Madarasa 82 ambayo yapo katika hatua mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, ni rai yetu kwa waheshimiwa Madiwani kuwaomba mkaziendeleze jitihada hizo ambazo zilifanyika katika Baraza lililopita kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi na ukamilishaji wa maboma hayo ili yatumike kwa ajili ya kukabiliana na upungufu nilioutaja hapo juu. Lengo ni kuhakikisha watoto wetu wanapata mahali stahiki pa kujifunza na kufundishia.

**2.11 Kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri katika kipindi cha robo ya kwanza 2020/2021 pamoja na taarifa za miradi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** baada ya mabaraza kusitishwa kwa muda ili kupisha uchaguzi mkuu, vivyo hivyo Baraza lako lilisitishwa. Katika kipindi hicho Timu ya Menejimenti iliendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muktadha huo katika mkutano huu wa kwanza wa Baraza, utapokea taarifa ya shughuli za maendeleo kwa kuzingatia sekta zilizo chini ya Kamati za Kudumu za Halmashauri kwa kipindi cha Julai mosi hadi tarehe 30 Septemba robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2020/2021. Vilevile, Taarifa ya Mapato na Matumizi pamoja na Mchanganuo wa shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hicho umeambatishwa katika makabrasha.

Hivyo, kwaniaba yangu mimi binafsi na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela naomba kwa heshima na Unyenyekevu mkubwa Baraza lako lizipokee taarifa hizi pamoja na Mihtasari ya vikao vya Kisheria vya Timu ya Menejimenti ya Halmashauri

IMC

[CMT] vilivyofanyika katika kipindi cha Julai – Oktoba 2020 kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

***Naomba kuwasilisha.***

John P. Wanga<br>
Mkurugenzi wa Manispaa<br>
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

IMC